

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

Simu. 028-2763213

028-2762534

Fax: 028-2763750

E-mail: Md@shinyangame.go.tz

Unapojibu Tafadhali Taja

Kumb. Na. SHY/MC/S.20/47/161

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa.

S.L.P. 28,
SHINYANGA.

Tarehe: 17/07/2017



YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya Msaidizi wa Hesabu (Accounts Assistant) nafasi hii ni kwa ajili ya kituo cha Afya cha Kambarage kilichopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga baada ya kupokea kibali chenye kumb.Na. AH/161/164/02/37 cha tarehe 21 Juni, 2017 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia kwa Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga kwa barua yenye kumb. Na. BA.83/97/01E/32 ya tarehe 29/06/2017.

1.0. MSAIDIZI WA HESABU (NAFASI 01).

(A) SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Awe na cheti cha kuhitimu nakufaulu kidato cha Nne (iv)
- ii. Awe na cheti cha ATEC level II au "Foundation level" kinachotambuliwa na NBAA.
- iii. Mwenye uzoefu wa zaidi ya mwaka mmoja katika fani hii atafikiriwa kwanza
- iv. Awe raia mwadilifu mtanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na 45.

B: KAZI/ MAJUKUMU:

- i. Kuandika na kutunza register" zinazohusu shughuli za uhasibu
- ii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
- iii. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki
- v. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana.

C: UWAJIBIKAJI:

- Atawajibika kwa Mweka Hazina wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

D: MSHAHARA:

- Atalipwa mshahara katika ngazi ya mishahara ya TGS "B" sawa na Tshs. 390,000/= kwa mwezi.

2. JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

- Barua zote ziandikwe kw amkono wa mwombaji nakutumwa kwa; Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Mansiapa ya Shinyanga, S.L.P. 28.


SHINYANGA.

3. MUHIMU:

- Mwombaji aliyewahi kupatikana kosa la jinai hatafikiriwa.
- Aidha barua ya mwombaji ionyeshe anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatanishwa na:
 - Maelezo binafsi ya mwombaji (CV)
 - Nakala ya vyeti vya shule na Chuo na Cheti cha kuzaliwa
- Weka picha mbili (2) za passport size
- Watakaoteuliwa kuhudhuria usaili (interview) watafahamishwa kupitia anuani walizotumia kwenye barua zao za maombi ya kazi.
- Testimonials na provisional results havitakubalika
- Nakala zote za vyeti vya shule. Chuo zipitie kwa Mwanasheria au Wakili yoyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa.

NB: Ajira hii ni ya Mkataba wa mwaka mmoja kulingana na Mkataba utakaopewa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 2/08/2017 saa 9.30 Alasiri.



Geoffrey Ramadhan Mwangulumbi

MKURUGENZI WA MANISPAA

SHINYANGA.

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA

NAKALA: i. Jalada: SHY/MC/S.20/47/161

ii. Mbao za Matangazo.